# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1021

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-842-2

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA SAIKOLOJIA NA SOSHOLOJIA YA ELIMU
# STASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU
## 2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023
Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-842-2

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kudurufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

Orodha ya majedwali ........ iv
Vifupisho ........ v
Shukurani ........ vi
1.0 Utangulizi ........ 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu ........ 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........ 2
3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu ........ 2
3.2 Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu ........ 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu ........ 2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4
6.1 Mkufunzi ........ 4
6.2 Mwalimu Tarajali ........ 4
6.3 Mzazi/mlezi ........ 5
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 5
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6
9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ........ 6
10.0 Idadi ya Vipindi ........ 7
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7
Bibliografia ........ 12

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Mwaka wa Kwanza na Mwaka wa Pili ........ 3

Jedwali Na. 2: Alama za Upimaji Endelevu ........ 7

Jedwali Na. 3: Maudhui ya mwaka wa Kwanza ........ 8

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Mwaka wa Pili ........ 11

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

**Shukurani**

Maandalizi ya muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala. Vilevile, Taasisi inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la maboresho ya Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu ni Somo la lazima katika Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Ujifunzaji wa somo hili utamwezesha mwalimu tarajali kuwa na uwezo wa kutumia misingi ya saikolojia na sosholojia ya elimu, kanuni na nadharia za ujifunzaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi. Aidha, somo hili litamwezesha mwalimu tarajali kutoa ushauri na unasihi kwa mwalimu tarajali ili kuwa na tabia na mienendo inayokubalika katika jamii. Vile vile somo hili litamwezesha mwalimu tarajali kuijua jamii yake na kujenga mahusiano chanya kati yake na mwanafunzi ili tendo la ufundishaji na ujifunzaji liweze kufikiwa kwa ufanisi.

Muhtasari huu umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa saikolojia na sosholojia ya Elimu ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu Tanzania Bara. Muhtasari unatoa maelekezo ya kuwawezesha mkufunzi kuandaa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu tarajali kwa ufanisi. Vilevile, muhtasari unatoa nafasi kwa wakufunzi kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ulimu.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba ili kuweza kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

Kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;

(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;

(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na

(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, classroom-based action research).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

Muhtasari wa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu unalenga kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;
(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;
(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;
(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (instructional leadership); na
(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, classroom-based action research)

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu una Umahiri Mkuu na umahiri Mahususi kama inavyojitokeza katika jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Mwaka wa Kwanza na Mwaka wa Pili*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu Saikolojia ya elimu katika ufundishaji na ujifunzaji | 1.1 Kumudu misingi ya Saikolojia ya elimu<br>1.2 Kuchambua hatua za makuzi na maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji<br>1.3 Kumudu nadharia na kanuni za ujifunzaji<br>1.4 Kumudu stadi za ushauri na unasihi kwa mwanafunzi |
| 2.0 Kumudu Sosholojia ya elimu katika ufundishaji na ujifunzaji | 2.1 Kumudu misingi ya Sosholojia ya elimu<br>2.2 Kuchambua masuala ya kijamii yanayoathiri malezi na ujifunzaji wa mwanafunzi |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji katika somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu unategemea ushirikiano baina ya Mkufunzi, Mwalimu tarajali na Mzazi/Mlezi katika kutimiza wajibu wao ambao ni:

### 6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki;

### 6.2 Mwalimu Tarajali

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ufundishaji na ujifunzaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia, kujifunzia na kutathmini mwanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

### 6.3 Mzazi/mlezi

Mzazi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika shughuli za ujifunzaji.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umejikita katika maarifa, stadi na mwelekeo. Mwalimu tarajali anatarajiwa kupata maarifa kuhusu elimu maalumu na kutumia muda mwingi kufanya mazoezi kwa vitendo kutokana na maarifa aliyoyapata. Mkufunzi unapaswa kutumia mbinu shirikishi zitakazomwezesha Mwalimu tarajali kujenga umahiri uliokusudiwa.

Elimu maalumu inapaswa kufanyika kwa vitendo zaidi ili kumwezesha mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika vitendo vya ujifunzaji na kukuza stadi za karne ya 21. Mwalimu anashauriwa kutumia mbinu shirikishi zitakazomwezesha mwanafunzi kujenga umahiri uliokusudiwa. Mbinu zinazopendekezwa kutumika ni pamoja na michezo, nyimbo, maigizo, ngonjera, uchunguzi, kazimradi, majadiliano, matembezi ya galari, mbinu ya kumualika mgeni, igizodhima na hadithi. Mwalimu anashauriwa kuwa mnyumbufu na mbunifu katika kutumia mbinu nyingine zinazoendana na mazingira husika ambayo ni rafiki na shirikishi kwa wanafunzi.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu, zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji ya ujifunzaji. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha mwalimu tarajali anapata nafasi ya kuona, kusikia na kushika zana bila kuathiri afya yake. Aidha, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa zimsaidie mwalimu tarajali kuelewa kinachofundishwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka. Zana za ufundishaji na ujifunzaji zilizopendekezwa ni pamoja na, matini zenye vifungu vya habari kuhusiana na saikolojia na sosholojia ya elimu, manila zenye taarifa za saikolojia na sosholojia ya elimu, chatipindu zenye maandiko ya saikolojia na sosholojia ya elimu, matini za kibunifu na zisizo za kibunifu kuhusu saikolojia na sosholojia ya elimu, michoro ya kisaikolojia, michoro mguso, picha, picha mguso, vitu halisi, kamusi zenye kufafanua mambo ya kisaikolojia na kisosholojia na kadi za alama za uakifishaji. Zana hizi zimependekezwa katika jedwali Na.3 la maudhui katika safu ya zana.

## 9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji ni suala muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya elimu utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Upimaji huu utamwezesha mkufunzi kupima umahiri wa mwalimu tarajali katika kumudu somo la Saikolojia na Sosholojia ya elimu. Aidha, utamwezesha mkufunzi kufuatilia kwa karibu maendeleo ya ujifunzaji ya mwalimu tarajali. Upimaji wa maendeleo utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Kwa hiyo, zana/vifaa vinavyotumika katika upimaji ni pamoja na mazoezi, maswali ya ana kwa ana, majaribio, hojaji, mkoba wa kazi, kazi mradi, na mitihani ya muhula.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Upimaji endelevu utachangia 30% na upimaji wa mwisho utachangia 70%. Aidha, mchanganuo wa alama za upimaji endelevu utakuwa kama ifuatavyo; Mtihani wa muhula wa kwanza utakuwa asilimia sita (6%), Mtihani wa mwisho wa mwaka wa kwanza utachangia asilimia sita (6%), Mtihani wa muhula wa kwanza mwaka wa pili utakuwa asilimia sita (6%). Kazimradi itakuwa asilimia saba (7%) na Mkoba wa kazi utakuwa asilimia tano (5%). Msimamizi tarajali wa karakana anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia 50% na upimaji tamati kwa angalau

kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafikisha 50%, msimamizi tarajali wa karakana anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Alama za upimaji zimeoneshwa katika Jedwali Na. 2

**Jedwali Na. 2:** *Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | Shughuli ya Upimaji | Mgawanyo (%) |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Muhula wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | Mtihani wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | Mtihani wa Muhula wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | Kazi mradi | 7.0 |
| 5 | Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| **Jumla** | | **30.0** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya elimu Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu, unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi viwili (2)

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu maalumu umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa vipengele sita ambavyo ni Umahiri mkuu, Umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali, vigezo vya upimaji, zana au vifaa vya kufundishia na kujifunzia na idadi ya vipindi. Majedwali yafuatayo yanaonesha Umahiri na Maudhui yanayopaswa kufundishwa katika ngazi ya Stashahada ya Ualimu somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu kwa mwaka wa kwanza na wa pili.

**Jedwali Na 3:** *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu Saikolojia ya elimu katika ujifunzaji na ufundishaji | 1.1 Kumudu misingi ya Saikolojia ya elimu | (a) Kuchambua dhana na misingi ya Saikolojia ya elimu *(maana, chimbuko, umuhimu na malengo)* | Dhana na misingi ya Saikolojia ya elimu umechambuliwa | Makala, Matini ya saikolojia Moduli, Picha na Michoro | 17 |
| | 1.2 Kuchambua hatua za makuzi na maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji | (a) Kuchambua hatua na nyanja za makuzi na maendeleo ya mwanafunzi na mahitaji yake ya msingi katika ufundishaji na ujifunzaji *(nadharia, nyanja, hatua na mahitaji)* | Hatua na nyanja za makuzi na maendeleo ya mwanafunzi na mahitaji yake ya msingi katika ufundishaji na ujifunzaji zimechambuliwa | Kadi za kliniki, Matini ya saikolojia Picha, Chati na Michoro | 17 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.3 Kumudu nadharia na kanuni za ujifunzaji | (a) Kuchambua nadharia na misingi ya ujifunzaji *(maana, nyanja, nadharia, kanuni, umuhimu na matumizi)* | Nadharia na misingi ya ujifunzaji vimechambuliwa kwa usahihi. | Makala,<br>Matini ya saikolojia<br>Moduli, Picha,<br>Michoro, na<br>Video za ushauri nasaha | 17 |
| | 1.4 Kumudu stadi za ushauri na unasihi kwa mwanafunzi | (a) Kuchambua nadharia, misingi na kanuni za ushauri na unasihi (*maana, nadharia, aina za unasihi, stadi za unasihi, umuhimu, tofauti* na *kanuni*) | Nadharia, misingi na kanuni za ushauri na unasihi zimechambuliwa kwa usahihi. | Makala,<br>Matini ya saikolojia<br>Moduli Picha,<br>Michoro, na<br>Video za ushauri nasaha | 17 |
| | | (b) Kuchambua kanuni za ushauri na unasihi kuhusu masomo na maisha ya kazi *(educational and career guidance and counselling)* | Kanuni za ushauri na unasihi kuhusu masomo na maisha ya kazi zimechambuliwa | Makala,<br>Matini ya saikolojia<br>Picha, Michoro na Video za ushauri nasaha | |

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana zinazopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | (c) Kuchambua miiko na maadili ya ushauri na unasihi (*sifa, maadili, miiko* na *umuhimu*) | Miiko maadili ya unasihi yamechambuliwa | Makala,<br>Matini ya saikolojia<br>Picha, Michoro na Video za ushauri nasaha | |

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Mwaka wa Pili*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu Sosholojia ya elimu katika ujifunzaji na ufundishaji | 2.1 Kumudu misingi ya Sosholojia ya elimu | (a) Kuchambua nadharia na misingi ya Sosholojia ya elimu (*maana, chimbuko, nadharia, umuhimu* na *malengo*) | Nadharia na misingi ya Sosholojia ya elimu imechambuliwa | Makala,<br>Matini ya saikolojia<br>Picha , Michoro na<br>Video za ushauri nasaha | 35 |
| | 2.2 Kuchambua masuala ya kijamii yanavyoathiri malezi na ujifunzaji wa mwanafunzi | (a) Kuchambua uhusiano wa shule na jamii katika malezi na ujifunzaji (umuhimu wa uhusiano wa shule na jamii na mchango wake katika uboreshaji wa malezi na ujifunzaji | Uhusiano wa shule na jamii katika malezi na ujifunzaji umechambuliwa | Vipeperushi,<br>Makala,<br>Matini ya saikolojia<br>Picha, Michoro na<br>Video za ushauri nasaha | 35 |

# Bibliografia


Barakett, J., & Cleghorn, A. (2000). *Sociology of education*: *An introductory view*. Prentice Hall.

Chattopadhyay, K (2022). *Sociology Of education*: *Theories and issues*. Kalpaz Publications

Feldman, R.S. (2019). *Essentials of understanding psychology (13th Ed.).* McGraw Hill.

Five H & Banes, N. (2022). *Educational psychology and transformational classroom*: *Research and theories*. Taylor & Francis

GaLbraith, V. (2017). *Counselling psychology.* Taylor & Francis

Hallahan, D. P., Kauffman, J. M. & Pullen, P. C. (2014). *Exceptional learners: An introduction to special education.* (12thEd). Pearson Education.

Kail, R. V. & Cavanaugh, J. C. (2016*). Human development*: *A life-span view.* Cengage

Kalat, J. W. (2017). *Introduction to psychology*: Cengage

Macintryre, C. (2010). *Play for children with special needs supporting children with learning difference 3*-9. Routledge

Mcleod.J & Mcleod J (2011). *Counselling skills. A practical guide for counsellors and helping professionals.* McGrawHill

Omari, I. M. (2006). *Educational psychology for teachers*. Dar es Salaam University Press.

Openstax College (2013). *Introduction to sociology.* Rice University

Peranglo, R. & Giuliian, G. (2008). *Teaching in a special education classroom: A step by step guide for educators.* Sage

Prout H.T & Fedewa A.L (2015). *Counselling and psychotherapy with children for scholl & clinical settings.* John Wiley and Sons, Inc.

Sanders, M. R., & Morawska, A. (2018). *Handbook of parenting and child development across the lifespan.*Springer. meetsteaching and learning

Tanzania Institute of Education (2013). *Diploma in Secondary Education Curriculum Module: Educational Psychology, Guidance and Counselling*. TIE